



... much more than  
a Bookshop

## TEXT BOOK CENTRE LTD

KIJABE STREET  
BOX 47540  
NAIROBI  
TEL. 330340/5  
FAX 225779



SARIT CENTRE, Phone 747405  
SPORTS & HOBBIES Phone 747406  
THE MALL Phone 441853

# WRITERS' forum

A Journal of  
the Writers'  
Association  
of Kenya  
Vol. 2, 1994

SHORT STORIES  
POEMS  
CRITICAL ESSAYS  
INTERVIEWS  
PROFILES  
REVIEWS



**THE JOMO KENYATTA FOUNDATION  
PUBLISHERS AND PRINTERS**

Get yourself a copy of the latest publications from JKF!

**BROKEN DRUM**

**DAVID G MAILLU**

By far the longest novel published in Africa, *Broken Drum* is a great story on cultural conflicts. Set in Nairobi Kenya, it spans several generations and is critical of the colonial past, the neocolonial present and the uncertain future. Compulsive reading for any one with a flair for some of the best writing from Africa's most prolific and best-selling author.

**BEYOND VIOLENCE**

**AGNES LEAKEY HOFMEYR**

A true story of hate, hurt and hope, *Beyond Violence* is Agnes Leakey Hofmeyr's personal story based on her early experiences in colonial Kenya and reaches its climax in the death of her father at the hands of the Mau Mau.

Agnes' story reads like a series of interesting anecdotes, but it is a book with a serious message for South Africa, one of forgiveness and reconciliation.

**WORLD OF ENCHANTMENT AND OTHER VERSES**

(POEMS FROM KENYAN SCHOOLS)

*World of Enchantment* is the first anthology of its kind and a testimony to the immense poetic talent in our school children a talent that has been taken for granted for too long. The poems display originality of thought, expression and imagination that make excellent reading.

**THE LAST HUNTER**

**DAVID G MAILLU**

The first in JKF's Pyramid Series, *The Last Hunter* is an exciting children's adventure story, set in the depths of the imaginary Makongo forest. Young Kimuyu finds himself twice lost in the hands of a mysterious spirit. Love wins the day as he is saved by (and saves) beautiful Maya.

Trade enquiries:

Jomo Kenyatta Foundation  
Sales and Marketing Department  
Enterprise Road  
P O Box 30533 (Tel 557222)  
Nairobi

# Contents

## Short Stories

|  |    |
|--|----|
| GIDEON MARETE: Saved by a Leopard .....              | 5  |
| WANJIRA MUTHONI: Why God Created Woman .....         | 10 |
| OMONDI MAK'OLOO: Love Made in Germany .....          | 19 |
| VALERIE CUTHBERT: Through Tired Eyes .....           | 26 |
| MWENDA MBATIAH: How to Tame the Sting of Death ..... | 29 |
| KYALLO WADI WAMITILA: Kituko Kijijini .....          | 32 |

|                    |    |
|--------------------|----|
| <b>Poems</b> ..... | 37 |
|--------------------|----|

## Critical Essays

|   |    |
|---|----|
| GITAARI NJUE: Language Choice and the Young Kenyan Playwright .....                       | 49 |
| SOPHIE W. MACHARIA: Perception of the Female Image in African - American Literature ..... | 56 |
| R.M. WAFULA: Uainisho wa Methali .....  | 62 |
| KITULA G. KING'EI: Swahili Taarab as a Medium of Political Expression in Kenya .....      | 74 |

## Interviews/Profiles

|  |    |
|--|----|
| MARJORIE OLUDHE MACGOYE: Interviewed by: Philo Ikonya<br>The Story of a Writer ..... | 93 |
| VALERIE CUTHBERT: Armchair Traveller .....   | 96 |

## Book Review

|  |     |
|--|-----|
| The Price of Liberty by: Paul Conton ..... | 101 |
| The Jail Bugs by: Wahome Mutahi .....      | 102 |

Published by

Writers' Association of Kenya  
C/O Department of Literature  
University of Nairobi  
P.O. Box 30197, Nairobi

©Writers' Association of Kenya and the authors

Contributions in this journal reflect the views of their authors and not necessarily those of WAK.

Typesetting and Printing by  
High Tech Computer Applies Agencies, P.O. Box 57995  
Nairobi

## Editorial

The Writers' Association of Kenya has come a long way. Like any other Association in our country, it has had its problems, but luckily for WAK, it has been able to solve many of its problems and survive as the foremost body in the vanguard of supporting and promoting literary creativity in the country. The publication of this second edition of *Writers' Forum* is yet another milestone in Kenya's literary history. It demonstrates, among other things, that literary creativity and incisive literary scholarship thrive in our country and, if tapped, they can bring out fresh and new understanding of literary phenomena. We do believe you will find these pieces valuable.

We are indebted to many people in the realisation of this dream. We take this opportunity to thank the Swedish International Development Agency (SIDA) for its continued assistance which has made possible the publication of the first and second issues of *Writers' Forum*.

If this issue brings to your literary awareness fresh knowledge and experience or if it tickles your creative instincts, great will be our pride!

Wanjira Muthoni  
Egara Kabaji

## Editorial Committee

|                   |                  |
|-------------------|------------------|
| Nana Wilson-Tagoe | Editor           |
| Kitula King'ei    | Assistant Editor |
| Wanjira Muthoni   | "                |
| Egara Kabaji      | "                |
| Kithaka wa Mberia | "                |
| Richard M. Wafula | "                |

## Uainisho wa Methali

### Utangulizi

Methali za lugha za Kiafrika zimeshughulikiwa na waandishi wengi. Kuna wale ambao wamezikusanya bila ya kuzifafanua wala kubainisha matumizi yake. Wengine wanazifafanua na kuonyesha jinsi zinavyotumiwa. Kitabu cha hivi karibuni zaidi kinachozungumzia methali kwa mapana ni **Kamusi ya Methali za Kiswahili** (1989) kilichoandikwa na Ahmed Ndal na G.K. King'ei.

Suala muhimu lililowakabili na kuzungumziwa na waandishi hawa, suala ambalo limegusiwa na waandishi na watafiti wengineo ni uainisho wa methali. Katika enzi hii tunamoishi, uainisho ni moja kati ya kaida zinazoliainisha somo kuwa la kitaalamu. Ujuzi mwingi wa wakati wetu unaelekezwa kwa vigezo na mielekeo ya kisayansi. Uainisho kama njia ya kulifafanua somo uliazimwa kutokana na masomo ya kisayansi kama Elimu-uhai na Kemia. Kwa ujumla, uainisho huliwezesha somo kuelezwa kwa uwazi, kwa namna inayofuatika, inayofasirika na kufahamika kwa urahisi. Mbali na uainisho bora kulifanya somo kuelezwa kimfumo, huwezesha vipengele mbalimbali vya somo hili kuhusishwa. Isisahaulike kwamba vitengo tofauti tofauti vya mfumo fulani huathiriana, kuingiliana na kutegemeana. Uainisho kwa mujibu wa **Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha** (1990) ni "ugawanyaji wa vitu katika aina zake kwa kufuata vigezo maalumu."

Methali zimegawanywa vipi? Kufungamana na fasili zinazoeleza maana ya 'methali' waandishi wengi kama Finnegan (1990), Parker (1974), Mattered (1987), Mulokozi (1989), King'ei na Ndal (1989) na Maitaria (1991) wamekubaliana kwamba methali ni matamshi yanayosheheni hekima na ambayo huwasilisha ujumbe wake kitamathali. Licha ya maelezo haya kueleza maana ya methali, hayamsaidii msomaji kufahamu aina za methali zilizopo. Na ugumu wa kutozifafanua methali katika makundi mbalimbali umeonyeshwa na King'ei na Ndal hasa wanaposema:

Katika kutalii fani ya fasihi kama methali, mtafiti hukumbana na shida kadhaa ambazo humkanganya. Kwanza, kwa vile wenyeji wa amali hizi hawakujaribu kuzipanga na kuzianisha fani hizi, ni vigumu kwa mtafiti

kuamua uainisho ufaao. Watafiti wengi hawakujali sana kuhusu maudhui na matumizi ya mafumbo haya hali hili ndilo jambo muhimu katika lugha ya fasihi (1989:IV)

Waandishi hawa wanawashambulia kwa upole wakisanyaji wa methali kama S.S. Farsi (1958) ambao walikusanya na kuziorodhesha methali kialfabeti bila kiambatisho chochote cha ufafanuzi. Tunakubaliana na maoni haya kwa ujumla. Shida ni kwamba licha ya kupewa mawazo haya ya kweli, waandishi hawa hawalijadili suala la uainisho kwa undani zaidi. Maoni yetu ni kwamba mawazo machache yanayotolewa katika dijabi hayatoshi kuelezea vigezo vinavyopaswa kutiliwa maanani katika ugawanyaji wa methali katika makundi mbalimbali.

### Matatizo ya Uainisho Uliopo

Lengo pana la makala haya ni kuonyesha kwamba methali hazijaainishwa kwa njia mwafaka, na kupendekeza njia nyingine ya kuzigawanya katika makundi mbalimbali. Imani yetu ni kwamba njia tutakayopendekeza ni bora zaidi. Ili umuhimu wa pendekezo letu uonyeshwe kinaganaga, inajuzu kupitia maandishi ya baadhi ya watafiti waliojaribu kuzigawa methali katika matawi tofauti tofauti<sup>1</sup>. B. Odaga na K. Akivaga (1982) wanazungumzia methali na vitendawili katika sura moja (uk. 110-115). Kutokana na maelozo yao, inaonekana kama tanzu hizi za fasihi simulizi ni ndogo sana. Hivyo basi, haziwezi kugawika zaidi katika matawi mbalimbali wala kujadiliwa kwa uketo. Pengine watafiti hawa wanaweza kusamehewa kwa kuwa wakati walipokuwa wakiandika, somo la fasihi simulizi katika shule za sekondari humu nchini lilikuwa halijashindilia mizizi yake. Marejeleo mengi yalihatijika shuleni pasi tahadhari kuchukuliwa kuhusu dosari zilizokuwemo. Si ajabu kwamba kitabu hiki kilichapishwa muda mrefu baada ya vitabu viwili tu kuandikwa, navyo vilikuwa *Kikuyu Folktales* (1970) na *Popular Culture of East Africa* (1972).

Shida moja ni kwamba tatizo hili linaendelezwa katika vitabu vinayofuatia. Katika kitabu alichokiandika Odaga (1984), Methali hazizungumziwi kwa njia ya kitaalamu. Anasema yafuatayo katika sehemu inayoshughulikia methali:

Hapa tuna methali ambazo tumezichagua kutoka katika jamii mbalimbali nchini Kenya. Baadhi ya methali ni rahisi na si ngumu kueleweka, zingine zinazusha hali ya utata. Kuna methali zinazopingana vilevile. (tafsiri yetu,

Matamshi haya yanamhamasisha msomaji kwa kumfanya atazamie ufafanuzi zaidi juu ya mitindo, miundo na matumizi ya methali rahisi, methali zinazotatanisha na hatimaye, methali zinazopingana. Kinyume na haya, Odaga anaanza moja kwa moja kuziorodhesha methali mia moja na kumi na mbili bila kuziambatanisha na kielezo chochote. Maoni yetu ni kwamba orodha kama hii haimsaidii msomaji kuzifahamu methali katika vitengo vyake vyote.

Mwandishi mwingine aliyefanya utafiti juu ya methali ni Naomi Kipury (1985). Kipury anashabihiana na Odaga kwa jambo moja, nalo ni kutoa orodha ya methali. Hata hivyo, anaiangalia mada yake kwa undani zaidi. Anatambua takriban aina thelathini na moja za methali. Aina hizi zinabainika kimaudhui. Nazo zinahusu:

- |   |   |  |
|---|---|--|
| 1. Dini, Mwenyezi Mungu na utukufu wake           | 10. Kutarajia na kujiandaa                      | 19. Undumakuwili                           |
| 2. Uhusiano wa kiukoo                             | 11. Maonyo juu ya kuwadunisha wengine           | 20. Ukaidi                                 |
| 3. Umoja  | 12. Mabadiliko ya nyakati na majira             | 21. Ng'ombe                                |
| 4. Bahati nzuri na majaliwa                       | 13. Maonyo kuhusu unafiki                       | 22. Umuhimu wa watoto                      |
| 5. Undaji na harakati za mtu dhidi ya unyonge     | 14. Hekima na ujinga                            | 23. Umilkaji na utegemeaji                 |
| 6. Matumaini na kukata tamaa                      | 15. Uvumilivu na ukosefu                        | 24. Kujipalia makaa                        |
| 7. Kuonya   | 16. Haki  | 25. Athari mbaya                           |
| 8. Kujiheshimu, kujigamba, wa uwezo na kutekeleza | 17. Kuwahi mapema na utaratibu mzuri wa kutenda | 26. Majivuno                               |
| 9. Usawa na ubaguzi                               | 18. Upinzani dhidi ya vita                      | 27. Ukweli na uwongo                       |
|   |   | 28. Sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu |
|   |   | 29. Hatima                                 |
|   |   | 30. Mambo bayana yanayohusu maisha ya mtu  |
|   |   | 31. Maisha kwa jumla                       |

Sifa nzuri ya kazi ya Kipury ni kwamba anajitathmini katika ziara yake ya kuzungumzia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Pamoja na kuziweka methali katika vikundi hivi, anakubali kwamba:

Katika mkusanyo huu, methali zimewekwa katika vikundi mbalimbali kulingana na dhamira zake. Tumefanya hivi ili turahisisha usomaji wa kitabu chetu. Methali zinafanana na ngano, vitendawili, nyimbo na ushairi kwa vile zote ni tanzu zenye maudhui yanayoingiliana (tafsiri yetu, uk. 149).

Jambo hili ni kweli hasa tukizingatia kikundi namba 29, 30 na 31. Vikundi hivi vinazungumzia kadhia zinazooingiliana, na pia, vinazungumzia nyinginezo zinazopatikana katika vikundi vingine. Kutokana na ukweli huu, tunabainikiwa kwamba matumizi ya vigezo vya kimaudhui kuainisha methali hayamwelekezi mtafiti kwenye ugawanyaji usiokuwa na utata.

Maelezo ya Kipury yanaonyesha kwamba utata haumo katika uainisho wa methali peke yake; umo pia katika ugawanyaji wa tanzu nyinginezo za fasihi simulizi kama ngano, tarihi, visakale, na visaasili. Mfano mmoja kutokana na uainisho wa ngano uliofanywa na Rose Mwangi utatosha. Mwangi anazigawa ngano katika makundi mawili. Zipo ngano zinazohusu wanyama. Miongoni mwa hizi, mna makundi mawili vilevile. Nayo ni ngano zinazohusu wanyama wajanja na zingine zinazoshirikisha majitu. Hatimaye, mwandishi anataeleza kwamba kadhia muhimu katika utambuaji wa ngano si vikale vya ujanja, ujinga wala ukatili bali ni mafunzo yanayotokana na ngano hizo (uk. 9).

Kanganyiko linalotokea hapa ni kwamba funzo laweza kukinzana na orodha ya vigezo vya mwanzo, ikiwa sasa hakuna njia maalumu ya kuzigawa ngano itayokubalika kuwa sahihi zaidi.

Madai yetu ni kwamba ijapokuwa kuna utata katika uainisho wa tagaa ndogo ndogo za fasihi simulizi, hii haimaanishi kwamba njia zinazoweza kutumiwa kusuluhisha utata huu zinafanana katika vipengele vyake vyote. Jambo muhimu chambilecho Abiola Irele (1981) ni kutumia njia zinazositisha utata. Katika makala haya tunashikilia kwamba uainisho wa kiisimu unafaa zaidi katika ufafanuzi wa methali.

## Vigezo vya Kiisimu

Hatudhamiri kuangilia uwanja wote wa isimu kwa vile hii ni taaluma pana sana. Tunalenga kuchukua baadhi ya sifa za Isimu zinazoweza kutuauni kufikiria kwa utaratibu zaidi kuhusu methali. Baadhi ya mawazo ya Ferdinand de Saussure na Roman Jakobson (1974) kuhusu lugha yatazingatiwa. Sifa bia za lugha pia ni muhimu katika kuzungumzia suala hili. Hatimaye isimuamali haiwezi kuepukika hasa pale ambapo tunawajibika kuzichanganua methali kutegemea maoni ya mtumiaji, vikwazo vya kijamii na athari za jamii juu ya matumizi ya methali hizo.

Kwa ujumla, muundo na maana ya methali ni mambo yanayofanana na muundo na maana ya lugha kama ilivyoelezwa na Ferdinand de Saussure. Muundo ni umbo la kitu kutokana na jinsi kilivyoundwa na kutengenezwa. Ingawa lugha ina mawanda matatu kwa mujibu wa maelezo ya De Saussure, tutatilia mkazo mawanda mawili pekee kwa kuwa haya yanahusu mada inayojadiliwa moja kwa moja. Sehemu mbili za lugha zinazodhihirika katika usemaji ni lugha dhahania na lugha tumikizi. Sehemu hizi za lugha zinafanana na miundo ya methali nyingi. Methali huelezea maana dhariri (lugha tumikizi) na maana batini (lugha dhahania). Kama ambavyo matumizi ya methali moja yanavyoweza kumulika nuru tajriba kochokocho za kijumla na kidhahania, lugha tumikizi pia inatupa fununu juu ya sifa kochokocho za lugha hiyo yenyewe kidhahania na kijumla. Katika makala haya, tutaonyesha hapo baadaye kwamba baadhi ya methali zina uwezo mkubwa zaidi wa kuwasilisha maana nyingi za kijumla kuliko methali nyinginezo. Jambo hili linaeleweka tukiingiza dhana ya tamathali ya usemi katika methali. Mtaalamu ambaye ameizungumzia dhana hii ni Roman Jakobson.

Jakobson anaiendeleza kazi ya De Saussure katika muktadha wa uhakiki wa ushairi. Anashughulikia lugha halisi na lugha ya kitamathali katika ushairi. Kimapokeo, lugha ya kitamathali hutumiwa badala ya maneno yaliyozowewa ili kutilia nuru na uthabiti jambo linalozungumzwa. Hali ipatikanayo katika matumizi ya stiari, kwa mfano, ni ubadilishanaji wa neno moja na neno jingine. Msingi wa ubadilishanaji huu ni kwamba kuna mshabaha wa kitajriba kati ya neno lililozowewa na lile la kitamathali. Tunaposema neno lililozowewa, tuna maana ya neno lisilohitaji tafsili husishi, neno linalopaswa kuchukuliwa kama linavyofahamika moja kwa moja na jamii-lugha fulani.

Kuna ubadilishanaji mwingine wa maneno unaoitwa metonimia: Katika metonimia, jina la sehemu ya kitu kimoja, au kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili. Mifano ifuatayo (Senkoro, 1982: 15) inathibitisha jambo hili:

|        |   |            |
|--------|---|------------|
| Jembe  | - | mkulima    |
| Kalamu | - | mwanafunzi |
| Ikulu  | - | Rais       |
| Mvi    | - | uzee       |
| Kiti   | - | uongozi    |

Jozi za maneno yaliyoandikwa hapo juu zinapatikana katika jamii moja kimuktadha. Baadhi ya maneno yanayopatikana katika jozi hizi yana uhusiano wa kimantiki, yaani moja linasababisha jingine. Uhusiano wa jembe na mkulima, kalamu na mwanafunzi ni wa kimetonimia. Neno la kwanza ni miongoni mwa sifa za neno la pili.

Badala ya kuzichukua dhana za metonimia na stiari kama dhana mbili tofauti zinazotumika katika mawanda mbalimbali ya maisha ya mtu, Jakobson anaitumia metonimia kuwakilisha lugha iliyozowewa na stiari kusimamia lugha ya kitamathali. Tofauti kuu iliyopo baina ya dhana hizi mbili ni kwamba metonimia siku zote huzungumzia kadhia zinazofahamika moja kwa moja ilhali stiari hueleweka tu baada ya kufasili na kutambua sifa zinazofanana kati ya mambo yanayolinganishwa. Tanzu mbalimbali za fasihi hutegemea uhusiano uliopo kati ya metonimia na stiari. Katika lugha ya kishairi kwa mfano, stiari na aina zingine za tamathali za usemi hubainika zaidi. Kwa upande mwingine, masimulizi ya kinathari hutumia uhusiano wa maneno kimetonimia kuwasilisha ujumbe wake. Maoni ya Jakobson ni kwamba umuhimu wa lugha ya kitamathali unalingana na wa lugha isiyokuwa ya tamathali. Kile ambacho lugha ya ushairi hufanya ni kumrusha msomaji katika malimwengu ambayo hajayazoea - na kumwezesha kuona tafsili nyingi za neno moja. Ukweli ni kwamba lugha ya binadamu yenyewe ni tamathali ya aina fulani kwa vile uhusiano uliopo baina ya neno na maana yake ni wa kunasibisha. Hivyo basi, lugha ya kishairi huzidisha ukengeushi wa msomaji kutokana na hali alizozoea.

Mawazo ya Jakobson yanaweza kumsaidia mtafiti wa methali kubainisha viwango vya "utamathali" vinavyopatikana katika methali tofauti tofauti. Kutokana na usaidizi huu, mtafiti anaweza kuzigawa methali kufungamana na matumizi ya lugha.

Maoni ya Jakobson yanarutubishwa na sifa bia za lugha. Miongoni mwa sifa bia hizi ni uwezo na lugha wa kufasiriwa kwa njia nyingi. Kiisimu, kuwepo na sanaa ni thibitisho kwamba lugha inaweza kuvyaziwa miundo mingi inayokubalika kadiri mtumiaji wake anavyotaka. Elizabeth C. Traugott na wengine (1981) wanasema kwamba lugha yaweza kuvivuka vizingiti vingi kimaana. Dhima kubwa ya washairi na wahakiki wa fasihi ni kubaini na kuchanganua utata kama kipengele kinachomwezesha

mwanasanaa kutumia maneno machache katika kuwasilisha maana pana.

Sifa bia nyingine ya lugha ni kwamba matumizi ya lugha hudhihirika zaidi katika muktanda maalum. Kila matamshi yana lengo au malengo. Na malengo haya ndiyo huzalisha miktadha ya matamshi fulani. Mbali na kuzingatia muktanda, matumizi ya lugha hutilia maanani mikatale, kaida na pengine mifumo ya kuzalisha mali ya jamii inayohusika. Kama tulivyowahi kutaja hapo awali, sehemu ya isimu inayotalii uwanja huu wa lugha ni isimu-amali.

Baadhi ya watafiti walioshughulikia uainisho wa methali wametumia vichache kati ya vigezo vya kiisimu bila kufafanua wazi kwamba wamevitumia. Waandishi wote walioziorodhesha methali na kisha kuonyesha matumizi yake wametilia maanani muktadha wa kijamii ambamo zinaweza kutumika. Hata hivyo waandishi hawa hawaonyeshi wazi iwapo muktadha ni kigezo cha aina yake cha kuzibainisha methali, au iwapo muktadha ni kiungo cha vigezo vya kiisimu.

## Mtazamo wa Methali Kiisimu

Kutokana na uchunguzi wetu kuhusu miundo na maana za methali na zadharia tuliyotumia, kategoria tatu muhimu za methali zinajitokeza. Kategoria ya kwanza inashirikisha methali zote zinazozingatia dhana ya Roman Jakobson kuhusu metonimia. Licha ya kwamba kimapokeo methali zimechukuliwa kubeba maana dhahiri na maana batini, kuna methali ambazo husheheni maana dhahiri zaidi kuliko maana fiche. Tunaweza kuzichukua methali hizi kuwa chanzo cha lugha ya kifasihi katika misingi ya metonimia.

Ukiziangalia methali zifuatazo kwa makini, utafahamikiwa na jambo tunalotaka kusema.

1. Asiyekuwapo na lake halipo.
2. Macho hayana pazia.
3. Hiari yashinda utumwa.
4. Auguwaye huangaliwa.
5. Heri kufa macho kuliko kufa moyo.
6. Hapana siri ya watu wawili.
7. Ikiwa hujui kufa, tazama kaburi.
8. Kazi isiyo kipimo mwisho watu huteta.
9. Waraka ni nusu ya kuonana.

Methali hizi zinazungumza kuhusu tajriba tofauti tofauti za maisha ya

binadamu. Jambo linalozifananisha zote ni matumizi ya lugha. Zinaweza kutumika kufafanulia hali ya maisha kimetonimia, pasi kuhitaji ufafanuzi zaidi. Maana za methali ni za dhahiri kama zinavyoonekana. Methali ya kwanza inaweza kutumika katika mazingira ambamo mnazungumzwa jambo linomhusu mtu asiyekuwapo. Methali ya pili inamaanisha kile kinachosemwa, yaani macho hayana pazia. Kama tulivyotangulia kusema, hizi ni methali zinazomaanisha lile linalosemwa na hapana haja ya kuzitafutia maana batini. Matumizi yake hutokea katika mazungumzo kufungamana na mtiritiko wa mazungumzo hayo moja kwa moja.

Kategoria ya pili ya methali ni ile ambayo pamoja na kujumuisha methali zinazowasilisha ukweli wa juu juu, husisitiza zaidi maana batini. Sababu ni kwamba maana zake dhahiri simeendelea kudidimia na kukabiliwa na ufinyu wa maana katika mapito ya wakati. Hili ndilo kundi kubwa zaidi la methali. Baadhi ya methali zinazopatikana humu ni:

1. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.
2. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
3. Simba mwenda kimya ndiye mla nyama.
4. Udongo uwahi ungali maji.

Katika methali ya kwanza, "mvungu" unaleta dhana ya juhudi nyingi zinapaswa kufanyika ili jambo litekelezwe. Kwa hivyo, ingawa maana ya awali ni kweli, maana hiyo imedidimia hivi leo kiasi kwamba, "Mtaka cha mvunguni" hufahamika kitamathali tu. Jambo jingine linamfunukia msomaji, nalo ni kwamba matumizi ya "mtaka cha mvunguni" hayakuwa ya kitamathali hapo awali. Maoni yetu ni kwamba wakati mmoja katika maisha ya mtu, methali zinazopatikana katika kategoria hii zilisheheni maana dhahiri peke yake.

Matumizi ya lugha ya kitamathali kama hii yanabainika pia katika stiari. Neno lililokuwa na maana halisi huweza kupewa maana nyingine nasibishi kutokana na tajriba zinazohusishwa nalo. Mfano mmoja utatosha. Katika mwaka wa 1975, ufisadi ulifanyika katika jumba la Water Gate huko Marekani, kwanza "Watergate" lilikuwa jina la mahali tu, kisha likatumika kumaanisha kosa la ufisadi lililofanywa na Rais wa Marekani wa wakati huo, Richard Nixon. Juzijuzi, sehemu ya jina la jumba hili imetumika kuashiria makosa mengine yanayofanana na kosa la awali. Huenda umekabiliana na "Irangate" na "Karanjagate" katika magazeti. Kutokana na mfano huu tunaweza kusesitiza kwamba katika kundi la pili ziwekwe methali zenye maana dhahiri na maana batini. Viwango vya "ufinche" vinaweza kuwa vingi. Lakini kila kiwango sharti kiwe na sifa zinazokishabihisha na

maana dhahiri.

Methali ya pili yaani "Usipoziba ufa utajenga ukuta" inaweza kufasiliwa katika njia mbalimbali kama:

- (i) Usipoziba ufa utajenga ukuta.
- (ii) Usipomfundisha mtoto tabia nzuri akiwa mdogo na akakosa mwelekeo unaofaa, hatimaye utajuta kwa kutompa mwenendo mzuri.
- (iii) Hali yoyote mbaya ikidhihirika, inapaswa kurekebisha mara moja kabla haijasakini.
- (iv) Usikubali kuchukua madeni mengi maana yakikushinda kulipa kwa hiari, utalazimika kuyalipa kwa gharama kubwa zaidi.

Mtiririko unaopiga mwangwi katika tafsili hizi zote ni onyo kuhusu kuepuka taabu kabla haijakuwa kubwa sana.

Tumesema kwamba methali zinazopatikana katika kundi hili zinaweza kusheheni viwango vingi vya ufiche. Kinachomaanishwa hapa ni kuwa methali nyingi zinazofanana kidhahania zinaweza kutumiwa kuleta fikra zinazofanana kidhahiri. Angalia mfano wa pili na wa nne katika kategoria ya pili: yote inaweza kutumiwa kudhihirisha hali halisi za maisha zinazofanana.

Kategoria ya tatu ya methali inahitaji ujuzi wa kimuktadha na kipragmatiki ili ieleweke. Hii ina maana kwamba juu ya maana za methali kutokana na malengo ya methali hizo katika mazungumzo maalumu, ufafanuzi wake utahitaji ujuzi wa itikadi, historia na kadhia nyinginezo zinazohusu Isimu-jamii ya watu wanaozungumziwa. Methali zifuatazo hazitatafsiliwa asilani ikiwa muktadha na masuala ya isimu-amali hayatiliwi maanani.

- (i) Ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona.
- (ii) \*Mwana mkaidi hafaidi mpaka siku ya idi.
- (iii) Ukistaajabu ya Mussa, utayaona ya firauni.
- (iv) Asante ya punda ni mateke.

Methali tatu za kwanza zinahusiana na utaratibu maalum wa maisha ya watu, hasa waislamu. Nayo methali ya nne inashughulikia uhusiano uliopo kati ya mfugaji na mifugo yake. Katika methali (I), mtu asiyeafahamu itikadi za kiislamu anaweza kufikiria kwamba, methali hii inawaasa watu kuwa makini katika uchaguzi wao wa vitu ili wajichagulie vile ambavyo ni vizuri zaidi. Anaweza kufikiria kwamba anayechagua nguruwe (pengine kwa ajili

ya kitoweo) anapaswa kumchagua aliyenona ili ala na ashibe.

Lakini ikikumbukwa kwamba Waislamu hawapaswi kula nyama ya nguruwe na ilhali methali hii imetokana na mazingira yao, hapana budi kwamba mtumiaji atabadilisha fikra zake kuhusu maana na matumizi yake ili aifungamanishe na itikadi za kiislamu ipasavyo. Ikiwa kula nyama ya nguruwe ni kukufuru, methali hii inalenga kukejeli. Pengine msikilizaji anaonywa kwamba asifanye kosa dogo akitazamia kuwa adhabu yake itakuwa ndogo vile vile. Adhabu za makosa yote, makubwa kwa madogo ni sawa. Hivyo basi, anayechagua kukôsa na afanye kosa hilo kwa mapana kwa kuwa adhabu ya mkosaji haitapunguzwa kwa kufanya kosa dogo. Tafsilihii ya kipragmatiki ni ya mwandishi na huenda ikakinzana na tafsili ya Waislamu wenyewe. La mno ni kwamba bila fununu za kipragmatiki, matumizi ya methali hii hayatafahamika.

Methali (2) pia inaweza kumpotosha mtumiaji ambaye hafahamu maana ya sherehe ya Idi. Anaweza kudhani kwamba maslahi ya mwana mkaidi hayalindwi kwa sababu ya mienendo yake isiyostahili. Kwa hivyo, katika mwaka mzima, mwana huyo atafaidika tu wakati wa sherehe ya Idi ambapo kila mtu ana furaha na huweza kumkaribisha yeyote, hata asiyejulika, ili washiriki pamoja katika sherehe. Kwa hakika, nilipata dhana hii kuhusu siku ya Idi nilipokuwa nikikaa Garissa. Hiyo ni siku ambapo majirani zangu (Waislamu) waliniarifu mapema kwamba sikutarajiwa kupika chochote kwa kuwa wangenigawia chakula. Sikudiriki kuona ukarimu mwingine wa aina hii mwaka wote isipokuwa siku hiyo maarufu ya Idi.

Fasili hii ilifaa kimuktadha kama nilivyoona wakati huo. Nionavyo sasa, maana ya kipragmatiki ya methali hii ni kinyume na imani yetu ya awali. Siku ya Idi hushirikisha baadhi ya mambo tuliyotaja hapo juu. Ulaji wa chakula si mchache. Ununuaji wa nguo mpya pia ni mwingi. Licha ya haya, mwana mkaidi hapewi wala kupata chochote. Hanunuliwi nguo mpya wala kupewa chakula kizuri. Mwana mkaidi "hukadiria faida" za tabia zake siku ya Idi. Kwa mujibu wa matumizi ya methali hii, siku ya Idi ni wakati wa kuzinyoosha tabia za vijana wenye mienendo mibaya.

Maana ya methali (3), "ukistaajabu ya Mussa utayaona ya Firauni", ni rahisi kueleweka kwa kuwa inalinganisha uwezo wa watendaji wawili. Hata hivyo, methali hii inawashangaza watu wanaofahamu mapokeo ya Kikristo na kiyahundi, na pia waliotelewa katika imani ya Kikristo. Kwa kawaida Myahudi na Mkristo wanaamini (kutokana na ithibati walizonazo) kwamba Musa alitenda maajabu mengi na makubwa zaidi kuliko firauni. Utendaji wa maajabu haya ulimlazimisha Firauni kuwacha huru Waisraeli. Ikiwa Firauni ndiye mtendaji wa vioja nivavyostaajabisha, lazima hoja hii imetokana na imani nyingine (isiyokowu ya kiyahudi wala ya kikristo). Hoja hii

imechimbuka kutoka Uislamu ambapo baadhi ya wahusika wanaotukuzwa katika Uyahudi na Ukristo wamedhalilishwa mbele ya wahusika wanaonasibishwa zaidi na Uislamu. Nimearifiwa na marafiki zangu waislamu kwamba aliyeponea chupuchupu kutolewa kama dhahibu hakukuwa isaka kama Wayahudi na Wakristo wanavyoamini bali alikuwa Ismail. Maelezo haya yanatuauni kujenga na kudhibitisha misingi ya kipragmatiki ya methali, (ukistaajabu ya Mussa..)

Methali ya mwisho katika orodha yetu ni ngumu kufasihiwa. Sababu ni kwamba ni nadra kwa punda kutarajia fadhila kutoka kwa binadamu. Katika hali ya kawaida, punda hubebeshwa mizigo mizito na binadamu. kwa hali na mali, punda humfaa binadamu. Punda anatazamiwa kupewa heko! Kinyume na haya, methali hii "inamlaumu" punda kwa kokosa fadhila.

Ili methali hii ifahamike ipasavyo, itikadi na mifumo ya uzalishaji mali ya jamii husika ni mambo yanayolazimu kutiliwa maanani. Pengine kimapokeo jamii hii ilikuwa na watumwa, na watumwa hao walitarajiwa kila mara kuwapongeza mabwana zao licha ya kutumikishwa kazi za shoko. Lakini wakati wa mapumuziko (fadhila ya "mfugaji" wa watumwa) ungefadhilisha mazingira ya kuzuka kwa maasi. Asante ya punda ni rahisi kueleweka katika hali halisi ya maisha. Huweza kutupa mateke wakati wa kupakuliwa mizigo..

## Tamati

Kutokana na nadharia na mifano ya methali tuliyotumia, inadhahirika kwamba ufasili na ufafanuzi wa methali kiisimu ni njia mwafaka ya kuzigawa methali katika makundi mbalimbali. Madai yetu ni kwamba sifa za lugha kama zilivyoenezwa na Ferdinand de Saussure na Roman Jakobson zinaweza kutusaidia kufikia uainisho wa methali unaotegemewa zaidi. Pendekezo letu ni kuwahimiza watafiti kutumia njia ya kiisimu kufafanulia methali za jamii mbalimbali.

## Tanbihi

1. Katika makala haya hatujishughulishi na uainisho wa tanzu pana za fasihi simulizi kwa kuwa jambo hili kitambo limefanywa na watafiti wengine kama Bascom na Ben-Dan Amos. Angalia Lindfors katika marejeleo.

2. Nimethibitisha jambo hili. Angalia **Koran**, Al-Saffat 37: 99-111.

## Marejeleo

- Balisidya, M.L. (1987), "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi" katika *Mulika Na 19*. Dar es Salaam. TUKI.
- Farsi, S.S (1958 ), *Swahili Sayings*. Nairobi: Kenya Lit. Bureau.
- Finnegan, R. (1970), *Oral Literature in Africa* London: Oxford University Press.
- Irele, A. (1981), *The African Experience in Literature and Ideology* London: Heinemann.
- Kapury, N. (1985), *Oral Literature of Maasai* Nairobi: Heinemann.
- Bernth Lindfors. (1977), *Forms of Folklore in Africa*. Austin London: University of Texas.
- Lo Liyong, T. (1972), *Popular Culture of East Africa*. Nairobi: Longmann.
- Maitaria, J. N. (1991), "Methali za Kiswahili kama chombo cha mawasiliano: Mtazamo wa kiisimu jamii," Tasnifu ya M.A , Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mulokozi, M.M. (1989), "Tanzu za Fasihi Simulizi" katika *Mulika Na 21* Dar es Salaamu: TUKI
- Mlacha, S.A.K (1985), "Dhima ya Methali katika Malezi" katika *Kiswahili*. 51/1 2 52/2. Dar es Saalam, TUKI
- Mwangi, R. (1970), *Kikuyu Folktales* Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Ndalu, A., G.K. King'ei (1989), *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: Heinemann.
- Odaga, B., K. Akivaga, (1982), *Oral Literature: A School Certificate Course*. Nairobi: Heinemann.
- Odaga, B. (1984), *Yesterday's Todays: The Study of Oral Literature*. Kisumu: Lake Publishers & Enterprises.
- Parker C.A. (1974), "Aspect of Theory of Proverb." Ph.D Thesis, University of Washington.
- Scholes, R. (1974), *Structuralism in Literature: An introduction*. New Haven & London: Yale University Press.
- Senkoro, F. E. M (1982), *Fasihi*. Dar es Saalam: Press & Publicity Centre.
- Traugot, L. & Wengine (1980), *Linguistic for students Literature*. New York: Brace Harcourt Jovanovich, Inc.
- TUKI, UNESCO & SIDA (1990), *Kamusi Sanifu na Isimu ya Lugha*. Dar es Salaamu: TUKI & Educational Publishers & Distributors Limited.